



## HALMASHAURI YA WILAYA YA KALIUUA

S. L. P 83 Kaliua, Simu: 0736204192

Nukushi: 0732988451, Barua pepe: ded@kaliuadc.go.tz

Tovuti: www.kaliuadc.go.tz

Barabara ya Kaliua/ Ulindwanoni

TAREHE: 21/03/2018

### **TANGAZO LA MNADA WA HADHARA WA MALI CHAKAVU PAMOJA NA NG'OMBE SIKU YA JUMANNE TAREHE 10/04/2018.**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua anawatangazia wananchi wote kuwa kutakuwa na mnada wa hadhara wa kuuza mali chakavu siku ya Jumanne tarehe 10/04/2018 kuanzia saa nne kamili (4.00) Asubuhi katika eneo la Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W) Kaliua. Mali hizo ni kama inavyooneshwa kwenye Jedwali hapa chini:-

<b>Na</b>	<b>Aina ya Mali</b>	<b>Namba ya Usajili</b>	<b>Mahali ilipo</b>	<b>Hali yake</b>
1	Nissan Patrol	SM 4139	Ofisi ya Mkurugenzi	Halitembei
2	Toyota Hilux D/Cabin	SM 3987	Ofisi ya Mkurugenzi	Halitembei
3	Toyota L/Cruiser Hardtop	SM 3426	Ofisi ya Mkurugenzi	Halitembei
4	Toyota L/Cruiser Hardtop	SM 3883	Ofisi ya Mkurugenzi	Halitembei
5	Pikipiki Suzuki	SM 4370	Ofisi ya Mkurugenzi	Halitembei
6	Pikipiki Suzuki	SM 4269	Ofisi ya Mkurugenzi	Halitembei
7	Pikipiki SANLG	T 362 AVP	Ofisi ya Mkurugenzi	Inatembea
8	Pikipiki SANLG	T 567 CGF	Ofisi ya Mkurugenzi	Inatembea

9	Pikipiki APOLO	T 146 BCC	Ofisi ya Mkurugenzi	Inatembea
10	Pikipiki LUHAO	MC 726 ABH	Ofisi ya Mkurugenzi	Inatembea
11	Baiskeli Sabini na moja (71)	-	Ofisi ya Mkurugenzi	Zinaridhisha
12	Jembe moja (1) la kukokotwa na ng'ombe (Plough)	-	Ofisi ya Mkurugenzi	Zinaridhisha
13	Mashine ya Kusaga nafaka	-	Ofisi ya Mkurugenzi	Inaridhisha
14	Ng'ombe 27	-	Ofisi ya Mkurugenzi	Nzuri

#### **MASHARTI YA MNADA.**

1. Mali hizo zitauzwa kama zilivyo na mahali zilipo.
2. Mnunuzi atatakiwa kulipa asilimia ishirini na tano (25%) ya bei hapo hapo na asilimia sabini na tano (75%) iliyobaki italipwa ndani ya siku kumi na nne (14) baada ya mnada. Endapo mnunuzi atashindwa kutimiza sharti hili, atakosa haki zake zote za ununuzi wa mali husika na amana itakayokuwa imelipwa haitarudishwa.
3. Mtu atakayetaja bei ya juu kisha akashindwa kulipa asilimia ishirini na tano (25%) ya bei aliyotamka atachukuliwa kuwa ni mwenye kuvuruga mnada na hivyo hatua kali zitachukuliwa dhidi yake kwa mujibu wa sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
4. Mali haitaondoshwa kwenye mnada isipokuwa tu kama kodi zote husika zitalipwa kikamilifu au kwa kibali maalum cha kamishna wa Forodha na Ushuru wa Bidhaa.
5. Mnunuzi atatakiwa kuondoa mali atakayonunua katika mnada ndani ya siku saba(7) kuanzia siku ya kukamilisha malipo.
6. Ruhusa ya kuangalia mali itakuwa siku mbili (2) kabla ya tarehe ya mnada.



**DKT. JOHN M. PIMA**

**MKURUGENZI MTENDAJI (W),**

**HALMASHAURI YA WILAYA KALIUA**

MKURUGENZI MTENDAJI  
HALMASHAURI YA WILAYA KALIUA  
KALIUA